22120300

International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

**SWAHILI A1 – STANDARD LEVEL – PAPER 2**
**SWAHILI A1 – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 2**
**SWAHILI A1 – NIVEL MEDIO – PRUEBA 2**

Tuesday 15 May 2012 (morning)
Mardi 15 mai 2012 (matin)
Martes 15 de mayo de 2012 (mañana)

1 hour 30 minutes / 1 heure 30 minutes / 1 hora 30 minutos

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Answer one essay question only. You must base your answer on at least two of the Part 3 works you have studied. You may include in your answer a discussion of a Part 2 work of the same genre if relevant. Answers which are not based on a discussion of at least two Part 3 works will not score high marks.
- You are not permitted to bring copies of the works you have studied into the examination room.
- The maximum mark for this examination paper is *[25 marks]*.

INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N’ouvrez pas cette épreuve avant d’y être autorisé(e).
- Traitez un seul sujet de composition. Vous devez baser votre réponse sur au moins deux des œuvres de la 3e partie que vous avez étudiées. Le cas échéant, vous pouvez inclure dans votre réponse une discussion sur une œuvre du même genre littéraire étudiée dans la 2e partie du programme. Les réponses qui ne sont pas basées sur au moins deux des œuvres de la 3e partie n’obtiendront pas une note élevée.
- Vous n’êtes pas autorisé(e) à amener des exemplaires des œuvres que vous avez étudiées dans la salle d’examen.
- Le nombre maximum de points pour cette épreuve d’examen est *[25 points]*.

INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Elija un tema de redacción. Su respuesta deberá basarse en al menos dos de las obras estudiadas en la Parte 3. Se podrán hacer comentarios sobre una obra de la Parte 2 del mismo género, si fuera necesario. Las respuestas que no incluyan una discusión sobre al menos dos obras de la Parte 3 no recibirán notas altas.
- No se permite traer a la sala de examen copias de las obras estudiadas.
- La puntuación máxima para esta prueba de examen es *[25 puntos]*.


© International Baccalaureate Organization 2012

*Jibu swali* ***moja*** *tu la insha. Jibu lako liegemee kwenye angalau kazi mbili za kazi za sehemu ya 3 ulizojifunza. Unaweza kuingiza katika jibu lako majadiliano ya kazi ya sehemu ya 2 ya utanzu huohuo ambao umejitayarisha nao. Majibu ambayo* ***hayana*** *mjadala wa angalau kazi mbili za sehemu ya 3* ***hayatapewa*** *alama nyingi.*

**Tamthilia**

**1.** Onyesha jinsi waandishi wa kazi mbili tofauti ulizozisoma wanavyowatumia wahusika katika kuendeleza maudhui yao wakitumia sifa na tabia zao.

**2.** Jadili jinsi waandishi wawili wa kazi mbili ulizozisoma wanavyotumia mbinu rejeshi katika kufanikisha kazi zao na uonyeshe jinsi wanavyoweza kuhusisha dhana hii katika kazi zao.

**Riwaya**

**3.** Onyesha vile mbinu simulizi inavyoathiri upitishaji wa ujumbe katika kazi mbili kutoka kwa waandishi wawili tofauti ulizozisoma.

**4.** Jadili vile matukio mbalimbali yanayojitokeza katika mazingira sawa yanavyotofautiana kwa sababu ya mbinu tofauti za lugha zinazotumiwa. Jadili ukizingatia kazi kutoka kwa waandishi wawili tofauti.

**Ushairi**

**5.** Ushairi ni midundo ya sauti au silabi zilizopangwa kwa ustadi na wasanii. Jadili kauli hii ukizingatia waandishi wawili wa kazi tofauti ulizozisoma ukionyesha vile mipangilio hii inavyochangia katika muundo na mtindo wa mashairi.

**6.** Ushairi ni njia moja ya kutoa wasio au ujumbe kwa njia iliyofupi na yenye utajiri mwingi wa lugha. Jadili ni kwa kiasi kipi na athari zipi wanashairi wanaweza kutumia lugha finyu ingawa yenye utajiri mwingi. Ukitumia kazi mbili za waandishi wawili tofauti ulizozisoma jadili kauli hii.

**Riwaya za mapenzi**

**7.** Onyesha vile waandishi wa kazi mbili tofauti ulizojitayarishia wanavyofaulu katika kutumia migogoro, mivutano na kusutana katika kuendeleza kazi zao.

**8.** Jadili vile waandishi wa kazi mbili ulizozisoma wanavyoweza kuzikuza hisia za wahusika wao zikiwa na uwezo na udhahiri.

**Maswala ya ujumla**

**9.** Fasihi hukuza sifa za wahusika kulingana na mchango wao katika kuendeleza maudhui ya mwandishi. Jadili ukizingatia kazi mbili za waandishi wawili tofauti ulizozisoma.

**10.** Kumhukumu mwandishi kama amefaulu katika kazi yake Kunategemea jinsi anavyotumia mbinu tofauti za lugha zinazowavutia wasomi wake. Jadili huku ukizingatia waandishi wa kazi mbili tofauti ulizozisoma.

**11.** Fasihi ni kama kasumba inayokolezwa kwenye akili za wasomi. Onyesha jinsi swala hili linavyozingatiwa na udhihirishe ukweli wake katika kukuza maudhui tofauti kwenye kazi za waandishi wawili tofauti ulizojitayarishia.

**12.** Katika kazi nyingi za fasihi, baadhi ya wahusika huchorwa wakiwa na uwezo au vyeo kuliko wengine. Ni kwa kiasi kipi swala hili linavyodhihirishwa kwenye kazi mbili za waandishi tofauti ulizozisoma?